MUNRASA WA 3 MITUEP UK2.

## Dk Mwinyi atilia mkazo uhuru wa kujieleza nchini



Unguja. Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi ameshauri mambo matano, likiwamo la kutumia Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari kama fursa ya kuweka mkazo wa uhuru wa kujieleza ndani ya ajenda ya jumla ya haki za binadamu... UK5

## Prof Jay: Madaktari wanatibu, Mungu anaponya



Dar es Salaam. Mwanasiasa na mwanamuziki nguli wa hip hop nchini, Joseph Haule ameelezea faraja aliyoipata baada ya mapokeo ya ujumbe wake kwa Watanzania... UK3

SUPA JACKPOT
TZS. 1,109,975,029
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

# MWANANCHI

TANZANIA Alhamisi, Mei 4, 2023 MWANANCH.CO.TZ ISSN 0856-7573 NA. 8299 BEI: TSH 1,000, KSH 60

# Joto uchaguzi 2025 Mbeya Mjini lapanda

*Swali la Mwakagenda kuomba jimbo hilo ligawanywe laibua mjadala, Chadema yaridhia ikisema itaharakisha maendeleo, Dk Tulia atajwa huku sifa stahiki zikiwekwa wazi*



"Serikali tunatambua, lakini nikuhakikishie, Mbunge wa Mbeya Mjini, ambaye ni Spika wetu Dk Tulia, ameshawasilisha suala hili na lipo mezani kwa hiyo muda utakapofika Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaitazama pia jimbo la Mbeya Mjini." Ummy Nderiananga



**37,591**
Idadi ya kura alizopata Sugu katika uchaguzi mkuu 2020 kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Ucahguzi (NEC).

"Mheshimiwa Waziri, Jimbo la Mbeya Mjini ni jimbo kubwa sana na lina kata zaidi ya 36 na wapigakura wengi, ni lini Serikali mtaamua kuligawa jimbo hilo ili liweze kuweka urahisi wa mbunge husika..." Sophia Mwakagenda



**75,225**
Idadi ya kura alizopata Dk Tulia na kutangazwa kuwa mbunge wa Mbeya Mjini katika uchaguzi wa 2020.



HABARI UK 4

## Siri Polisi kufuta leseni 3,000 za madereva, tinted marufuku UK 22

## Waziri Ulega amshukia Mpina UK 3





**250** Aina ya samaki na viumbe wengine wanaopatikana katika Ziwa Tanganyika huku maarufu zaidi wakiwa ni migebuka na dagaa maarufu kama dagaa wa Kigoma.

**90** Idadi ya siku ambazo shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika zitasimama ili kutoa fursa kwa samaki kuzaliana, uamuzi ukihusisha nchi nne.

# Hofu yatanda Ziwa Tanganyika kufungwa

HABARI UK 2

CamScanner

UVUVI HARAMU

# Hofu sasa yatanda Ziwa Tanganyika kufungwa

Happiness Tesha, Mwananchi
htesha@mwananchi.co.tz

**Kigoma.** Zikiwa zimebaki siku 11 kabla ya Tanzania kuanza kutekeleza makubaliano ya rasimu ya kusimamisha shughuli za uvuvi wa Ziwa Tanganyika kwa kipindi cha miezi mitatu, wavuvi, wasafirishaji wa mazao hayo na wabunge wamebaki njiapanda wakiomba Serikali itazame upya uamuzi huo.

Makubaliano ya kusimamisha shughuli hizo yalifanyika katika kikao kilichofanyika mwaka jana kikihusisha nchi zinazozunguka ziwa hilo ambazo ni Zambia, Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Nchi hizo zilikubaliana kanuni moja ya kutambua zana haramu za uvuvi ili kuruhusu mazalia ya samaki kwa wingi na kudhibiti uvuvi haramu, uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

Hata hivyo, alipoulizwa jana kwa simu, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema leo atakuwa na mkutano na viongozi wa mikoa na wilaya husika, wakiwamo wabunge kujadili utekelezaji wa suala hilo.

"Tunakwenda kujadiliana namna ya utekelezaji au vinginevyo. Tutapata uelekeo kesho (leo)," alisema Ulega.

### Kujengewa uwezo

Awali, katika kikao kingine cha kuwajengea uwezo maofisa wanaoshughulika na usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa nchi zote nne, kilichofanyika mjini Kigoma Februari 12, 2023, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya ziwa Tanganyika, Tusanga Sylvain alisema makubaliano ya kufunga ziwa hilo yalikuja mara baada ya kupokea malalamiko ya wavuvi ya kupungua kwa mazao ya uvuvi kutokana na uvuvi haramu.

Sylvain alisema nchi zote zimesaini makubaliano hayo na kwamba ikifika tarehe husika iliyokuwa imepangwa nchi hizo zitaweza kutekeleza na kuchukua hatua za kusitisha shughuli za uvuvi katika ziwa hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu.

> "Niwahakikishe ndugu zangu hakuna sababu yoyote ya kupata taharuki.Kesho (leo) tuna mkutano na wakuu wa wilaya zote na wabunge hilo neno ushirikishwaji tunakwenda kulimaliza kesho tunakaa tunajadili.
>
> Waziri Abdallah Ulega

### Kilio cha wavuvi

Akizungumzia hatua hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Wavuvi Tanzania, Francis John alisema kabla ya kusitishwa kwa shughuli za uvuvi Serikali ingewapa mikopo na elimu ya ufugaji wa vizimba vya samaki ili wakati wakisitisha shughuli wao wanaendelea na maisha ya uvuvi.

John ambaye pia ni Mwenyekiti wa vyama vya ushirika wa wavuvi Mkoa wa Kigoma, alisema ilipaswa wapate mikopo ya riba nafuu ili wafuge na kuendelea kuvua na kula samaki.

Alisema uvuvi haramu ni hali ya kutumia zana za uvuvi zisizoruhusiwa kisheria kuhatarisha mazalia ya viumbe hai vinavyoishi majini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wavuvi na wadau wa uvuvi mkoani Kigoma, wamesema kufungwa kwa ziwa hilo kutazorotesha hali zao kiuchumi kutokana na asilimia kubwa ya wakazi wa mkoa huo kutegemea ziwa hilo kimapato.

Mchuuzi wa samaki, Beatrice Simon alisema miaka mitano iliyopita alifiwa na mume wake lakini kupitia ziwa hilo amekuwa akipata mahitaji ya familia yake na kwamba endapo wataamua kusitisha shughuli ndani ya ziwa hilo kwa kipindi cha miaka mitatu hali ya maisha itakuwa mbaya kwao.

Kwa upande mwingine Mkurugenzi wa kampuni ya Mkungu Fish Export, Jamilu Alfan alisema walipopokea taarifa hizo waliambiwa na Serikali kuanzia Januari, 2023 watapewa mafunzo maalumu yatakayowasaidia wakati ziwa hilo litakapositishwa shughuli zake kwa miezi mitatu.

Alfan alisema Mei imeshaanza na kwamba hadi sasa hakuna kilichofanyika na hata wao hawajui hatima yao na kama wangearifiwa mapema wangeweza kuweka hata akiba ya mazao hayo.

Naye Meneja wa kampuni ya Lambati Fish Export, Asha Ibrahim alisema zaidi ya kampuni 20 za usafirishaji zitapoteza nguvu kazi za vijana endapo shughuli za ziwa hilo zitasitishwa na kuna uwezekano mkubwa wa matukio ya kiuhalifu kuongezeka katika mji wao kutokana na vijana wengi kupoteza ajira.



Wachuuzi wa dagaa katika Manispaa ya Kigoma Ujiji wakianika baada ya kuvuliwa. Picha na Maktaba

### SABABU YA KUZUIWA

Uamuzi wa kufunga ziwa hilo ulianza kusikika kutokana na kikao cha wadau wa uvuvi kilichofanyika Februari 24, 2023, mjini Kigoma kilichokuwa na lengo la kuwasilisha rasimu ya sensa ya vyombo vya uvuvi, ikiwemo idadi ya mialo, idadi ya wavuvi na aina ya zana pamoja na ukubwa wake.

Katika kikao hicho, Ofisa mfawidhi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi kanda kuu ya Ziwa Tanganyika, Juma Makongoro alisema ziwa hilo litafungwa kuanzia Mei 15, hadi Agosti 15, mwaka huu baada ya uvuvi haramu kuongezeka.

"Mei 2023 Tanzania itaanza kutekeleza makubaliano ya rasimu ya kusimamishwa kwa shughuli za uvuvi wa ziwa Tanganyika kwa kipindi cha miezi mitatu ikiwa ni makubaliano yaliyofikiwa katika kikao cha mwaka 2022 na nchi nne zinazozunguka ziwa hilo," alisema Makongoro.

Alisema mikakati ya Serikali kwa sasa ni kutoa elimu kwa wavuvi ya kuwa tayari na ziwa hilo linatarajia kufungwa kwa miezi mitatu na kuwawekea miundombinu bora, ikiwemo kuwashauri jinsi ya kufuga samaki wa bwawani



Wafanyabiashara wa samaki katika soko la Kibirizi kwenye Manispaa ya Kigoma Ujiji, Amina Sadiki (kushoto) na Halima Ramadhani (kulia) wakipaa samaki kabla ya kwenda kuwauza sokoni hapo. Picha na Maktaba

### Wabunge wang'aka

Suala hilo liliibuka bungeni jijini Dodoma jana, wakati wabunge wanaotoka mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa wakichangia mjadala wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2023/24, wakiitaka Serikali kuwa makini na jambo hilo.

"Mkoani Kigoma kuna taharuki sana kuhusu kufungwa kwa ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu kuanzi Mei 15. Ni jambo jema nikiwa kama mwakilishi wa wananchi sikusudii kupinga nalo isipokuwa ushirikishwaji wa wananchi unahitajika," alisema Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kilumbe Ng'enda.

Aliendelea, "kama hakuna ushirikishaji wa wananchi kunakuwa na ubatili, turudi kushirikisha wananchi."

Kwa upande wake, Mbunge wa Nkasi Kaskazini (Chadema), Aida Khenan aliunga mkono hoja ya Kilumbe Ng'enda akisema mikoa hiyo inasubiri tamko la Serikali.

"Ziwa Tanganyika tuna share nchi nne, DRC inatumia 45, Tanzania asilimia 41, hizo nchi mbili asilimia inayobaki ndiyo wanatumia.

"Unapoingia makubaliano ya kufunga na nchi zenye asilimia ndogo, lengo ni nini? Unakwenda kumnufaisha nani? Kama wengine wanaweza kuzungumzia korosho ndio uchumi wao, madini ndio uchumi wao, uchumi wetu ni Ziwa Tanganyika, ndio duka letu," alisema.

Alishauri Serikali kupambana na uvuvi haramu badala ya kukimbilia kusema kufunga ziwa.

Naye Mbunge wa Kigoma Kusini (CCM), Nashon Bijanguze, mbali na kulalamikia kutoshirikishwa, alisema hadi sasa Serikali haijatoa ajira mbadala kwa wavuvi.

"Nimekwenda kufanya ziara kwenye kata mbili, Sigunga na Mgambo, Sigunga wameniambia, mbunge tunaomba kama ziwa linakwenda kufungwa tuandalie makaburi, hatuna kazi nyingine ya kufanya kazi yetu ni hapo ziwani. Hiyo kauli ni nzuri kwa wananchi ambao ni wapiga kura?

Suala la kutoshirikishwa pia limelalamikiwa na Mbunge wa Viti maalum Mkoa wa Kigoma (CCM), Sylvia Sigula akisema,"haiwezekani leo bado siku nane, sisi wawakilishi hatuna taarifa rasmi kuhusu kufungwa kwa ziwa."

Wakati mbunge huyo akiendelea kuzungumza, Mbunge Ng'enda alitoa taarifa akisema Bunge la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imekataa hoja ya kufunga ziwa Tanganyika, "kwa maana hiyo, leo (jana) tuko kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano na sisi tunakataa."

### Majibu ya Waziri Ulega

Kuhusu ziwa Tanganyika Ulega alisema "limesemwa kwa kirefu sana kuhusu Ziwa Tanganyika kufungwa na wabunge wa Kigoma, Rukwa, Katavi, wamesema kwa mapana na wananchi wamewasikia na sisi tumewasikia," alisema Ulega.

Alisema wa suala hilo ulikuwa na lengo jema lakini haikulazimisha nchi wanachama namna ya kutekeleza itifaki kwa kufanana.

CamScanner

MWANANCHI UK 3.



...seph Haule
...kwenye
...uru
...a hapa nchi-

...wa wataal-
...ani. Asante

...wa Utama-
...Michezo,
...a 'Mwana-
..."Mungu ni

...wa Ser-
...igwa ame-
...ezi Mungu
...risha zaidi
...biri mitul-

...nguli wa
...Mbilinyi
...ita amean-
...Mungu ni
...ataendelea
...ni wazi ana
...wa bado na

...kutoka
...aliandika:
...Keep the
...huku Dia-
...akiandika
...a."
...ya Korog-
...elo alian-
...ema sana.
...wa ujasiri
...ve ni shu-
...ke wa Pro-
...a."
...is Sultan
...le tuna-
...unapata
...maisha
...ntihani
...ma ni
...ame-

# Waziri Ulega amshukia Mpina

**Habel Chidawali**, Mwananchi
hchidawali@mwananchi.co.tz

Dodoma. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema wizara imejipanga kufanya mabadiliko makubwa, huku akisema upimaji wa samaki kwa kutumia rula aliousimamia bosi wake wa zamani, Luhaga Mpina haukuwa sahihi.

Ulega alisema hakukusudia kumjibu Mpina kwa kuwa wakati samaki wanapimwa yeye (Ulega) alikuwa naibu waziri lakini alibaini kulikuwa na upungufu, kwa sababu hiyo hakuweza kumkosoa bosi wake huyo wa zamani.

Upimaji wa samaki kwa rula ulifanywa mwaka 2018 na mtumishi wa wizara hiyo aliyejulikana kwa jina la Komakoma katika kantini ya Bunge, wakati huo Mpina alikuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Jana jioni, Ulega akihitimisha hotuba ya bajeti yake alisema upimaji huo haukuwa sahihi kwa kuwa samaki aliyepimwa alikuwa amekaangwa, kitaalumu alishapoteza uhalisia wake, jambo ambalo lisingeweza kumpa majibu ya uhalisia.

"Nataka niseme na msema kweli ni mpenzi wa Mungu, kwa nini huwa sisemi kuhusu rula iliyopima samaki pale kantini, ni kwamba kitaalamu samaki akishapikwa anapoteza shepu na mwonekano, kwa hiyo majibu hayawezi kuwa ya uhakika.

"Mheshimiwa Spika, alitaka nimwambie mzee hapo unapotea, sikumwambia hivyo, sikugombana naye na ndiyo maana mimi Abdalah Ulega niko hapa kwenye podium (mimbari) labda ningegombana naye ningeambiwa sina adabu nagombana na viongozi wangu na nisingekuwa hapa," alisema Ulega.

Kuhusu uchomaji wa vifaranga, alikiri kweli sheria inasema hivyo, lakini ndani ya sheria kuna kitu kinachoitwa busara na kilichopo ni uchomaji wa hadharani na ndiyo tatizo.

Awali, Mpina ambaye ni mbunge wa Kisesa (CCM) alitaka Serikali ieleze sababu za kutosema uchomaji wa vifaranga na upimaji wa samaki uliofanyika kwa mujibu wa kanuni ya 58 ya uvuvi ya mwaka 2009.

Hata hivyo, Mpina alijikuta kwenye wakati mgumu alipotakiwa kupeleka uthibitisho baada ya kumtaja Waziri Mkuu amekuwa akitoa maelekezo lakini hayafanyiwi kazi na waliochini yake, jambo alilosema linasababisha upungufu.

Mchango wake ulimuibua Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro aliyeomba kumpa taarifa akieleza mbunge huyo alitumia vibaya jina la Waziri Mkuu kwa madai maagizo ya kiongozi huyo yanatekelezwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama alisema mchango wa mbunge huyo ulituhumu mtu ambaye maagizo na maelekezo yake yameanza kufanyiwa kazi na watumishi, wakiwamo mawaziri ndani ya Serikali.

Mpina alipopewa nafasi alisisitiza anao ushahidi wa anachokisema, hivyo anaweza kupeleka ushahidi huo kama akiombwa.

Kutokana na hilo, Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson alisema ili atoe uamuzi wa mwongozo huo, itampasa Mpina kupeleka ushahidi huo kwanza, ingawa hakusema ni muda gani atatumia kuupeleka kwake.

**"Nataka niseme na msema kweli ni mpenzi wa Mungu, kwa nini huwa sisemi kuhusu rula iliyopima samaki pale kantini, ni kwamba kitaalamu samaki akishapikwa anapoteza shepu na mwonekano, kwa hiyo majibu hayawezi kuwa ya uhakika."**

Ulega



CamScanner